



KARABEY COMPANY LIMITED

P.O BOX 11814, MWANZA , TEL +255 990 470

MKATABA WA KUPANGSHA ENEO LA OFISI PAMOJA NA YARD WA TAREHE 01/01/2025

Mkataba huu ni baina ya KARABEY COMPANY LIMITED

ambae katika mkataba huu anatambulika kama **mpangishaji/mmiliki** wa eneo husika.

NA

GEO GULF DRILLING SOLUTIONS wa P.O BOX 11615, MWANZA

ambae katika mkataba huu anatambulika kama **mpangaji** wa eneo husika.

Katika mkataba huu imekubaliwa

1. Kwamba mpangishaji atampangisha mpangaji jengo moja la ofisi pamoja na eneo lililo nyuma ya ofisi hiyo kwa ajili ya matumizi ya yard katika eneo lililo linamilikiwa na mpangishaji. **SABASABA, ILEMELA MWANZA**

2. Kwamba, mpangaji ameliona eneo hilo na ameridhia kuwa linamfaa kwa matumizi ya kazi zake

3. Kwamba, **GHARAMA ZA KODI** ya upangishaji wa eneo hilo ni **MILIONI MBILI NA LAKI NNE (2,400,000/=Tsh)** kwa **MWAKA**

3. Kwamba gharama zote za uboreshaji wa eneo hilo ili liendane na matakwa ya mpangaji atazibeba mpangishaji mwenyewe na zitatokana na kodi itayolipwa.

4. Gharama zote za maji, umeme, ulinzi na gharama ambazo ziko nje na makubaliano haya zitakua juu ya mpangaji mwenyewe.

5. Kwamba Kuanzia tarehe ya kuanza mkataba huu hadi tarehe ya kuisha kwa mkataba huu, eneo hilo litakua chini ya mpangaji.

6. Kwamba katika kipindi chote cha mkataba huu, mpangaji atalitumia eneo hilo kwa shughuli halali na tulizokubaliana katika maongezi na si kwa shughuli zilizozo zuliwa kwa mujibu wa sheria za nchi yetu.

HIVYO BASI

1. **MPANGAJI** amelipa jumla ya **SHILINGI MILIONI TISA NA LAKI SITA (9,600,000/= Tsh)** ikiwa ni gharama za upangaji wa eneo hilo kwa **KIPINDI CHA MIAKA MINNE** kuanzia tarehe 01/01/2025 hadi tarehe 01/01/2029

2. **MPANGISHAJI** amekubali mpangaji atumie pesa za kodi hiyo ya miaka minne kutengeneza ofisi na baada ya miaka minne mpangaji ataanza kulipa kodi mpya ambayo itakuwa na ongezeko la asilimia 10 kwa Mwaka.

3. **MPANGISHAJI** amemkabidhi eneo **MPANGAJI** tayari kwa maboresho na matumizi husika.

4. **KWA KUTIA SAINI** katika mkataba huu pande zote mbili zimekubaliana na yote yaliyo katika mkataba huu.

Kwa niaba ya **KARABEY CO. LTD**
NAME: RASHID ABDALLAH ALLY
POSITION : DIRECTOR
DATE: 01/01/2025



SIGN: 

Ikishuhudiwa na
NAME: *NASSER ABDULLAH ALY*
POSITION: *DIRECTOR*
DATE: 01/01/2025

SIGN: 

Kwa niaba ya **GEO GULF DRILLING SOLUTIONS**
NAME: ANWAR ABDALLAH ALLY
POSITION: DIRECTOR
DATE: 01/01/2025



SIGN: 

Ikishuhudiwa na
NAME: SULTAN NASSER AL SAAD
POSITION: DIRECTOR
DATE: 01/01/2025

SIGN: 